THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KCPE 2016

## KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma Maagizo Yafuatayo Kwa Makini.)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzoni mwa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1–50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**
   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **21.** Chagua jibu lenye ala za muziki pekee.
   A. filimbi, udi, mvukuto, chapuo
   B. njuga, tari, kinubi, fidla
   C. harimuni, marimba, msondo, maleba
   D. siwa, zeze, upatu, nembo.

   Jibu sahihi ni B.

   **Katika karatasi ya majibu:**

   1 [A] [B] [C] [D] 11 [A] [B] [C] [D] 21 [A] ~~[B]~~ [C] [D] 31 [A] [B] [C] [D] 41 [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.
10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

906504

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**
*© The Kenya National Examinations Council 2016*

**Geuza Ukurasa**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Umuhimu wa afya bora kwa raia __1__ , __2__ kuna wasiotilia maanani suala hili. Raia __3__ afya hawamudu __4__ kukabiliana na matatizo __5__ maisha, __6__ pia huwa na hamu zaidi ya kutenda kazi. Raia wanastahili kuhimizwa kutunza afya __7__ wasije wakahasirika baadaye kwani, __8__.

1. A. utakuwa umesisitizwa   B. umekuwa ulisisitizwa
   C. unakuwa umesisitizwa   D. umekuwa ukisisitizwa

2. A. ama   B. japo   C. wala   D. lau

3. A. wenye   B. zenye   C. kwenye   D. penye

4. A. tu   B. kamwe   C. kabisa   D. hata

5. A. yanaodhuru   B. yanavyodhuru   C. yanayodhuru   D. yanakodhuru

6. A. au   B. bali   C. na   D. hata

7. A. nao   B. hao   C. zao   D. wao

8. A. rasharasha ndio mwanzo wa mvua   B. tone na tone huwa mchirizi
   C. maji ukiyavulia nguo yaoge   D. mchelea mwana kulia hulia mwenyewe

Sitawahi kumsahau Bi. Tunu; __9__ hamu ya kujiendeleza masomoni. Nakumbuka kidato cha kwanza nilipokuwa __10__ katika Kiswahili. __11__ somo kuwa rahisi. Alitufunza aina za mashairi kama vile __12__ lenye mishororo mitano katika ubeti. Alisisitiza kwamba ushairi ni mwepesi, Akasema, "Ikiwa mtoto mdogo anaweza kutunga na kukariri shairi __13__ nyinyi __14__" Pia, Bi. Tunu alitufundisha aina za tamathali za usemi kama vile, sitiari. Mfano wa sitiari ni __15__.

9. A. ndiye aliyenipa   B. ndivyo alivyonipa
   C. ndipo aliponipa   D. ndio alionipa

10. A. nimeenda shoti   B. nimekula mwande
    C. nimeenda nguu   D. nimekula hasara

11. A. Aliifanya   B. Uliifanya   C. Alililfanya   D. Ulililfanya

12. A. tathnia   B. takhmisa   C. tathlitha   D. tasdisa

13. A. madhali   B. ilhali   C. angalau   D. sembuse

14. A. ;   B. ,   C. ?   D. .

15. A. Mkai anawaza akiwazua kila siku.   B. Hamira ni ninga anayetuliza.
    C. Kitambaa hiki ni laini kama pamba.   D. Mawimbi ya bahari yalinizungumzia.

*Kutoka swali la **16** mpaka **30**, chagua jibu lililo sahihi.*

**16.** Chagua sentensi sahihi kisarufi.
A. Nywele ambayo imesukwa ni fupi.
B. Ngome iliyojengwa hapa imetukinga.
C. Jino iliyooza imeng'olewa na daktari.
D. Changarawe ambacho kimesombwa kitauzwa.

**17.** Ukigawanya nusu mara nne sawa utapata?
A. robo B. sudusi
C. khumusi D. thumni

**18.** Chagua jibu lenye sauti sighuna pekee.
A. ch, f, s, th B. gh, j, m, t
C. p, ny, n, d D. dh, k, ng', h

**19.** Nomino **nyanja** imo katika ngeli gani?
A. U–ZI B. I–ZI
C. I–I D. LI–YA

**20.** Maneno yaliyopigiwa mstari ni: Sesi alibeba vikapu <u>kadha begani</u>.
A. kielezi, kiwakilishi;
B. kivumishi, kihusishi;
C. kiwakilishi, kihusishi;
D. kivumishi, kielezi.

**21.** Chagua jibu la kitendawili kifuatacho. Mimi ninakula vyakula vyote vinono lakini sinenepi wala sikui.
A. ulimi na meno;
B. kinu cha kusagia;
C. chungu cha kupikia;
D. mkono na vidole.

**22.** Onyesha usemi halisi wa sentensi ifuatayo. Muli aliniambia kwamba wiki ambayo ingefuata angeenda kutazama mechi hiyo.
A. "Wiki ambayo ilifuata nilienda kutazama mechi hiyo." Muli akaniambia.
B. "Wiki ijayo nitaenda kutazama mechi hiyo." Muli akaniambia.
C. "Wiki ambayo ilipita ulienda kutazama mechi hiyo." Muli akaniambia.
D. "Wiki ijayo utaenda kutazama mechi hiyo." Muli akaniambia.

**23.** Nukta pacha hutumiwaje?
A. kutanguliza maneno katika orodha;
B. kufungia maneno halisi ya msemaji;
C. kuonyesha ufafanuzi wa maneno ya ziada;
D. kubainisha maneno ya awali.

**24.** Ni jibu lipi sahihi?
A. Utaridi ndiyo sayari iliyo karibu sana na jua.
B. Zebaki ndiyo sayari kubwa zaidi ya zote.
C. Zuhura ndiyo sayari angavu yenye joto zaidi.
D. Mshtarii ndiyo sayari iliyo karibu zaidi na dunia.

**25.** Chagua sentensi iliyotumia kiunganishi sahihi.
A. Fauka ya kumwita alikataa kuitika.
B. Maadamu umeniomba nitakusaidia.
C. Maria alijaribu bighairi akashinda.
D. Umu ni msomaji bora ikiwa hanivutii.

**26.** Maana ya nahau, "tia mrija" ni:
A. kutumia mali vibaya;
B. kumtegemea mtu kwa kila kitu;
C. kujitafutia mali kwa hila;
D. kumchukulia mtu mali ya mwenzake.

**27.** Ni jibu lipi lenye maelezo sahihi?
A. Mzegazega huuza bidhaa rejareja.
B. Saisi hutunza wanyama wa uchukuzi.
C. Mjume ni fundi wa kufua visu.
D. Sogora ni fundi wa kuimba na kukariri mashairi.

**28.** Chagua kauli ya kutendewa ya sentensi hii. Malkia alipiga ngoma akiwa kwa Hamu.
A. Ngoma ilipigiwa kwa Hamu na malkia.
B. Malkia alipigiwa ngoma kwa Hamu.
C. Ngoma ilipigiwa Hamu na malkia kwake.
D. Malkia alipigiwa ngoma na Hamu kwake.

**29.** Chagua wingi wa sentensi ifuatayo. Jani hilo kavu lilipeperushwa likatua kwenye mlingoti.
A. Majani hayo makavu yalipeperushwa yakatua kwenye mlingoti.
B. Majani yale makavu yalipeperushwa yakatua kwenye milingoti.
C. Majani yale makavu yalipeperushwa yakatua kwenye mlingoti.
D. Majani hayo makavu yalipeperushwa yakatua kwenye milingoti.

**30.** Ni jibu lipi lenye methali zenye maana sawa?
(i) Mzigo uko kichwani kwapa lakutokeani jasho?
(ii) Pilipili usiyoila yakuwashiani?
(iii) Mtama usioula wawawingiani kuku?
(iv) Kuku alaye mtama atakuwaje na nyama?
A. (i), (iv) B. (ii), (iii)
C. (i), (ii) D. (iii), (iv)

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali* **31** *mpaka* **40**.

Wanafunzi wengi hudhani kwamba michezo ya riadha huanzia shuleni. Hata hivyo, ukichunguza kwa makini utapata kwamba watu huanza kushiriki katika riadha na michezo mingine wakiwa watoto wakembe. Ikiwa unakumbuka vyema, utapata kwamba ulianza kucheza kabumbu mara tu ulipoanza kutembea. Mara ya kwanza mpira wako ulikuwa sahani ya mama yako, au hata kikombe ulichotiliwa maziwa. Ulipokua kiasi, wewe na wenzako mliunda mpira kwa karatasi, majani au vitambaa, ambavyo mara nyingi mliokota kwenye majalala.

Huenda unakumbuka mara yako ya kwanza kuogelea. **Sitashangaa ukiniambia kuwa kidimbwi chako kilikuwa maji machafu yaliyokuwa nje ya nyumba yenu**. Wengine wataniambia kuwa waliogelea kwenye vijito vilivyojaa konokono **bila kuwa na mwao** na hatari ya kuambulia magonjwa. Licha ya kuogelea, wewe na wenzako pia mlishiriki katika michezo mingine kama vile kurusha tiara, kibe, kuwinga kuku na ndege kwa mawe, kuvutana kwa kamba, kuruka kamba, na kuzungushia tairi kwenye kiuno. Wakati mwingine mlikimbizana ili kuona anayempiku mwenzake.

Ukiulizwa kuhusu michezo mliyoshiriki mkiwa watoto, utasema kwamba michezo hii mliitunga wenyewe. Kadhalika nyinyi wenyewe ndio mliotunga sheria ambazo zilidhibiti uchezaji wenu. Wale ambao walivunja sheria hizi walipewa adhabu kali kama vile kutengwa na kikundi au kupewa kazi ya kuwahudumia wengine wakiendelea kucheza. Bila shaka adhabu hizi ziliimarisha nidhamu miongoni mwenu. Hali kadhalika michezo hii yenu haikuwaleta pamoja tu, bali pia ilichangia kuimarisha urafiki. Mathalani, mmoja wenu alipoumia, kundi zima lilimshughulikia. Aidha, michezo hii ilikuza ubunifu na ujasiri. Kule kutengeneza mipira na nyavu kwa nyasi au karatasi kuliwapa stadi zaidi za kuunda hata vifaa vikubwa zaidi. Vilevile ni wazi kwamba ulipoirusha tiara yako, na kuwashinda wenzako katika mbio, ulijihisi kuwa shujaa na kujiamini zaidi. Wakati mwingine hata ulichaguliwa kuwa kiongozi wa kundi kutokana na umahiri wako katika michezo.

Natumai unafahamu kuwa michezo hiyo yenu iliwasaidia kujenga misuli na kuimarisha viungo vya mwili. Ni wazi kwamba wakati uliposhiriki michezo hii ulijihisi mwepesi zaidi, na uliweza kutekeleza mengi bila kuchoka haraka. Zaidi ya hayo, michezo hiyo ilikuwezesha kupata usingizi wa pono na kuraukia shule bila kulazimishwa na mlezi wako. Ikumbukwe kwamba michezo hiyo hiyo ndiyo inayoendelezwa hata shuleni. Manufaa yake ni mengi hata kwa watu wazima. Wanaoshiriki michezo hii katika nyanja za kieneo na kimataifa hujifaa kwa mengi. Kuna wale ambao hushinda tuzo na nishani mbalimbali kutokana na weledi wao. Wengine hupata fedha nyingi na kuambulia utajiri wa ghafla. Pia baadhi huteuliwa kuchezea timu za kimataifa na kuziletea familia, na nchi yao sifa kuu. Wapo wanaoajiriwa kama makocha na marefa wa timu za kitaifa na kimataifa.

Mke ni nguo, mgomba kupaliliwa. Nao utendaji wako katika michezo unahitaji kuboreshwa kila mara. Ushauri wa walimu na wanajamii wengine ni muhimu katika kukuimarisha michezoni. Hao hukuelekeza kuhusu namna ya kuutumia muda wako vyema; usije ukaegemea sana katika michezo ukasahau mengine muhimu kama vile kudumisha usafi, kuzingatia masomo na mahusiano ya kifamilia. Kadhalika, ni sharti ufuate nasaha ya waelekezi wako kuhusu njia bora ya kutumia pato ambalo huenda ukapata kutokana na michezo.

**31.** Kulingana na aya ya **kwanza**:
A. Watoto wanapofika shuleni hawajui michezo ya nyumbani.
B. Wanafunzi wanaojihusisha na riadha huwa wachanga.
C. Watoto huimarisha uchezaji kutokana na vifaa kwenye mazingira yao.
D. Wanafunzi hupata jinsi ya kujifunza kulingana na wanavyokua nyumbani.

**32.** Kifungu kimebainisha kwamba:
A. Watu wanapowaza kwa dhati huelewa wanavyoanza.
B. Watoto wakitembea wakicheza hawajui umuhimu wa vitu.
C. Mpira ukiundwa kwa karatasi huchezewa jaani.
D. Watu wanapohitaji jambo hutafuta mbinu za kulifikia.

**33.** '**Sitashangaa ukiniambia kuwa kidimbwi chako kilikuwa maji machafu yaliyokuwa nje ya nyumba yenu**,' ina maana kuwa:
A. Msomaji anajua kuwa aliogelea mwanzo kidimbwini.
B. Mwandishi ana imani kuwa nyumba ina maeneo machafu.
C. Msomaji anaamini kuwa anaambiwa kuhusu uogeleaji kule nje.
D. Mwandishi ana hakika kwamba watoto walichezea maji yale.

**34.** Kulingana na aya ya **pili**:
A. Viumbe wa majini huwaumiza wagonjwa wanaoogelea.
B. Msomaji anakumbuka alipoanza kurusha tiara nyumbani.
C. Wenzako walijificha mlipowafukuza ndege na kuku.
D. Michezo mingine ya watoto ilisababisha ushindani.

**35.** Kulingana na aya ya **tatu**:
A. Mtu asiyejua sheria michezoni hawezi kuhurumiwa.
B. Watu wakiwa pamoja huunda mikakati ya kudumisha mahusiano mema.
C. Huduma bora hutolewa na wanaokosea michezoni.
D. Michezo huwapa watu ujasiri wanapowashughulikia wagonjwa.

**36.** Michezo:
A. inapowaleta watu pamoja idadi ya marafiki huwa nyingi nyumbani
B. ikiendelea kundini huzidisha matayarisho ya kazi
C. inawafanya watu kuwa na moyo wa kukabiliana na magumu
D. inasababisha kuwepo kwa mashabiki kunakorushwa tiara.

**37.** Kulingana na kifungu:
A. Wanafunzi wanakuwa viongozi wanapoona ubora wa michezo.
B. Mtu anayeshiriki michezo hupata utulivu zaidi wa mwili.
C. Misuli huimarika mtu anapofahamu umuhimu wa kucheza.
D. Viungo hujengekea michezoni mtu anapofanya kazi kwa urahisi.

**38.** Chagua jibu sahihi kulingana na kifungu.
A. Walezi hawawaamshi watoto wanaopenda michezo.
B. Faida za michezo shuleni huwa nyingi ikianzia nyumbani.
C. Watu wazima wakichezea timu za kimataifa huajiriwa.
D. Kushiriki michezo huweza kuimarisha hali ya mtu kiuchumi.

**39.** Kulingana na aya ya mwisho, '**mke ni nguo, mgomba kupaliliwa**', kwani
A. Mchezaji akielekezwa vyema huweza kutumia riziki yake kujinufaisha.
B. Mwanafunzi akifuata ushauri wa mwalimu huzingatia chanzo cha familia.
C. Mtu akishiriki michezo vyema huweza kufikia udumishaji usafi.
D. Mtoto akihusika vyema katika familia hupata njia ifaayo ya kujiimarisha.

**40.** Maana ya '**bila kuwa na mwao**' kulingana na kifungu ni', bila:
A. kufahamu
B. kuamini
C. kuogopa
D. kuajabia

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali* **41–50**

Meli alipokivuka kizingiti cha lango la shule ya kitaifa ya Tungambele alikuwa na azma ya kusoma kwa bidii ili kuinukia kuwa kijana wa kutegemewa na jamii yake. Alikuwa kalelewa katika familia yenye pato wastani. Akasoma kwa juhudi za wazazi wake hadi darasa la nane alipokwangura alama za kumwezesha kujiunga na shule hii ya kifahari. Meli alijua kwamba alikuwa mwanagenzi, si katika masomo ya shule ya upili tu, bali pia katika maisha ya jijini ambamo shule hii ilipatikana. Kwa kweli hii ndiyo iliyokuwa mara yake ya kwanza kutia guu kwenye jiji hili ambalo habari zake akizisoma, ama katika magazeti machache yaliyowahi kufika kijijini mwao, au kupitia soma la Elimujamii. Hata hivyo, Meli hakuwa mtu wa kuogopa au kunywea machoni mwa changamoto. Alijiambia kwamba kwa vyovyote vile atapambana na maisha haya mapya.

Saa mbili kamili asubuhi ilimpata Meli kapiga foleni katika afisi ya kuwasajili wanafunzi wageni. Wasiwasi wa aina fulani ulianza kumnyemelea alipotazama hapa na pale bila kuona dalili ya mja yeyote aliyemfahamu. Alijihisi kama yule kuku mgeni ambaye mwalimu wake alishinda kuwaambia kuwa hakosi kamba mguuni. Hata hivyo uliupiga moyo wake konde na kujiambia kuwa kuja kwake hapa kulitokana na juhudi zake mwenyewe na katu hatauruhusu ugeni wa mazingira kuifisha ari yake ya masomo.

Usajili ulikamilika, naye Meli na wenzake wakajitosa katika ushindani wa kimasomo jinsi waogeleaji wajitumbikizapo kidimbwini wakapiga mbizi, baadhi wakiambulia ushindi na wengine wakifedheheka kwa kushindwa. Meli na wenzake walibainikiwa kwamba wote walikuwa mabingwa kutoka majimbo na wilaya zao. Ilimbidi kila mmoja wao kujikakamua zaidi ili kuelea katika bahari hii ya ushindani. Muhula wa kwanza ulishuhudia kishindo cha Meli kubwagwa chini na majabali wenzake. Alijipata miongoni mwa wanafunzi kumi wa mwisho; au kama alivyozoea **kuwatania** wenzake katika shule ya msingi, "wanafunzi kumi bora kuanzia mwisho"! Hili lilimwatua moyo Meli na kumfanya kutahayari. Alifika kwao amejiinamia kama kondoo aliyeumia malishoni. Akawataka wazazi wake wambadilishie shule lakini wakakataa.

Muhula wa pili na wa tatu mambo yalikuwa yaleyale. Meli akahisi kama askarijeshi aliyeshindwa kabisa kutambua mbinu za kuwavizia maadui. Akaona kwamba njia ya pekee ni kujiunga na wenzake kama yeye katika vitendo vya utundu kama vile kuvuruga masomo kwa kupiga kelele darasani, kupiga soga bwenini na hata kuvuta sigara. Mwanzoni alichukia vitendo hivi lakini alimeza mrututu akisema kwamba ndiyo njia ya pekee ya **kujipurukusha** na aibu. Wazazi wa Meli hawakusita kutambua mabadiliko katika hulka ya mwanao. Wakajaribu kumshika sikio nyumbani lakini akawa hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Wakawahusisha wataalamu wa nasaha ambao waliwaambia kuwa Meli hakuwa na tatizo lolote la kuyamudu masomo. Kile alichokosa ni kujiamini tu.

Wazazi wa Meli waliona kuwa ni muhimu kuwahusisha walimu katika kutatua tatizo la mwanao. Mwanzo wa muhula wa pili uliwapata wazazi hawa afisini mwa naibu wa mwalimu mkuu. Mazungumzo kati ya wazazi, naibu wa mwalimu mkuu na mwalimu wa darasa la Meli yalidhihirisha kwamba walimu walikuwa wamemuasa Meli kuhusu kujiingiza katika makundi yasiyomfaidi lakini rai zao ziliingia katika masikio yaliyotiwa nta. Aliyopenda zaidi Meli ni shughuli zilizomtoa nje ya shule kama vile tamasha za muziki, ukariri wa mashairi na drama. Mazungumzo yalibainisha kwamba Meli alihitaji ushauri na uelekezaji zaidi kutoka kwa mtaalamu wa nasaha pale shuleni.

Meli alianza vikao na mtaalamu huyu ambaye pia alimpendekezea Meli ushauri zaidi kutoka kwa washauri marika. Hili lilimchangamsha zaidi Meli kwani aliwaona hawa kama wenzake waliojua changamoto zake. Juhudi za mtaalamu wa nasaha na washauri marika zilifua dafu. Mwisho wa kidato cha pili ulishuhudia mabadiliko makuu katika hulka na utendaji kimasomo wa Meli. **Aliukata kabisa uhusiano wake na marafiki waliompotosha** na kuanza kuandamana na wanafunzi waliotia juhudi masomoni. Polepole alama zake ziliimarika. Matokeo ya mtihani wa kidato cha nne yalimweka kwenye safu ya wanafunzi bora zaidi nchini.

**41.** Nia ya Meli katika elimu ilikuwa:
A. kuinua hali ya familia yake;
B. kuisaidia jamii yake;
C. kupata alama nzuri;
D. kujiunga na shule bora.

**42.** Meli alipojiunga na Tungambele:
A. alifahamu machache kuhusu uanagenzi;
B. alijua machache kuhusu masomo ya upili;
C. alifahamu machache kuhusu jiji;
D. alijua machache kuhusu maisha mapya.

**43.** Kifungu kimedhihirisha kwamba:
A. Tungambele iliwasajili wanafunzi bora zaidi katika maeneo yao.
B. Wanafunzi walijitolea kwa bidii ili wasifedheheke.
C. Meli na wenzake walijua ni mabingwa siku waliposajiliwa.
D. Watu walitazamana kwa woga walipoanguka mitihani.

**44.** Kulingana na kifungu:
A. kutofikia malengo kunaweza kusababisha kuzorota kwa maadili;
B. kutofanya vyema darasani kunaweza kusababisha kubadilishwa shuleni;
C. kuanguka katika masomo kunaweza kunyima njia za kujiokoa;
D. kupoteza alama kunaweza kuzua upigaji wa kelele.

**45.** Chagua jibu **lisilo** sahihi kwa mujibu wa kifungu.
A. Meli alivuta sigara na kupiga soga ili kujisahaulisha unyonge wake.
B. Wazazi wa Meli walikuwa wenye makini.
C. Meli hakutambua umuhimu wa masomo.
D. Wazazi wa Meli walitambua haja ya kushirikiana katika malezi.

**46.** Kulingana na aya ya **tano**:
A. Meli alikuwa bingwa katika ukariri wa mashairi na drama.
B. Tabia ya Meli iliathiriwa vyema na marika zake.
C. Wataalamu wa nasaha shuleni ndio waliojua tatizo la Meli masomoni.
D. Walimu walikuwa wamemwonya Meli dhidi ya upigaji soga na uvutaji sigara.

**47.** Kulingana na kifungu, ushauri marika unafaa zaidi kwani:
A. anayeshauriwa hujitambulisha zaidi na washauri;
B. washauri hupendekezwa na wataalamu;
C. anayeshauriwa anaelewa zaidi matatizo yake;
D. washauri huwafurahisha wanaoshauriwa.

**48.** "**Aliukata kabisa uhusiano wake na marafiki waliompotosha**". Chagua kauli inayoweza kujumuisha maneno haya.
A. Aliuacha ubaharia kwa unahodha.
B. Aliliacha ganda la muwa la jana.
C. Aliukata mkono uliokuwa ukimlisha.
D. Alimtupa jongoo na mti wake.

**49.** Maana ya: **kuwatania** ni
A. kuwafanyia dharau;
B. kuwafanyia chuku;
C. kuwafanyia mzaha;
D. kuwafanyia inda.

**50.** Chagua maana ya: '**kujipurukusha**', kwa mujibu wa kifungu.
A. kujiokoa;
B. kujisahaulisha;
C. kujilinda;
D. kujiepusha.